


245



KIBABII UNIVERSITY

UNIVERSITY EXAMINATIONS

**2020/2021 ACADEMIC YEAR
FOURTH YEAR SECOND SEMESTER**

MAIN EXAMINATION

FOR THE DEGREE OF BACHELOR EDUCATION (ARTS)

COURSE CODE: KIS 405

COURSE TITLE: EDITORIAL METHODS IN KISWAHILI

DATE: 13/10/2021

TIME: 2:00PM-4:00PM

INSTRUCTIONS

Answer **three** questions **only**.

Question **one** is **compulsory**.

Time: Two (2) Hours

KIBU observes ZERO tolerance to examinations cheating

Maswali

1. a). Tumia alama kuhariri kifungu kifuatacho.

(alama 10)

Bara la Afrika limekuwa likijitahidi kuinua kiwango chake cha maendeleo. Hata hivyo, maendeleo ya Afrika na juhudi zake zinazolenga kufikia ufanisi yanategemea matumizi ya lugha za kiasili hasa iwapo juhudi hizo zinawalenga wakazi wa mashambani (Prah, 2008). Ingawa Maendeleo haya yanategemea matumizi ya lugha za kiasili, kuna wale wanaopinga matumizi ya lugha hizo. Watu hawa hawawanadai kwamba wasikilizaji wa lugha za kiasili ni wachache. Kwa mfano, wote Soyinka akiwa kati ya wanaopinga matumizi ya lugha za kiasili, anamshutumu mwandishi Ngugi wa Thiongo kwa kuandika vitabu vyake kwa lugha ya kikikuyu. Kwa mujibu wa Wote Soyinka, hali hiyo inapunguza idadi ya wasomaji ambao huenda wasielewe lugha hizo za kiasili (Ongarora, 2002).

Mitazamo hasi kama hiyo ya Wote Soyinka ni ya kusikitisha kwani maendeleo katika uandishi wa habari, uchapishaji, utalii na kadhalika yatapanuka zaidi ikiwa lugha za

Kiafrika na tamaduni zitapewa nafasi kukua na kuchangia maendeleo (Muthwii, 2002). Maendeleo hayo yatafikiwa, iwapo lugha za kiasili zitatumika zaidi si tu katika uandishi bali pia katika vyombo vya habari. Kutokana na matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari, idadi kubwa zaidi ya walengwa wa habari zinazohusiana na jamii husika zitaweza kufikiwa. Hivyo basi, kwa vyombo vya habari zinazowasilishwa kupitia zitakuwa za manufaa zaidi hususan kwa wananchi walioko mashinani iwapo lugha za Kiafrika zitatumika.

Hapa nchini Kenya, redio imetumika kama kifaa cha kushughulikia mahitaji ya watu mbalimbali kama vile upashaji habari na burudani. Kwa miaka mingi, mbinu zinazolenga mawasiliano zimetumika kama njia ya kushughulikia masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi (Gathigi, 2009). Kuhusu masuala ya kijamii, redio inadaiwa kuleta ukuruba mkubwa miongoni mwa wasikilizaji. Redio imewaleta pamoja wasikilizaji kupitia vipindi kama vile vya kutumiana salamu redioni.

b) Fafanua vigezo vyovyote vinne vinavyopaswa kuzingatiwa katika uteuzi wa picha katika taaluma ya uhariri.

(alama 8)

- c) Kwa kutumia mifano, ainisha makundi yoyote matatu ya wachapishaji. (alama 6)
- d) Elezea athari zozote tatu zinazoweza kujitokeza kutokana na wizi wa haki za kumiliki. (alama 6)
2. Wewe ni afisa wa uajiri katika shirika la uchapishaji la Baraka. Njuguna ameajiriwa kama mhariri mdogo wa shirika hilo. Kwa kutumia mifano, mpe majukumu anayopaswa kutekeleza katika wadhifa wake huo wa mhariri. (alama 20)
3. a) Kwa kutumia mifano, fafania haki zozote tano za kiuchumi anazopaswa kuzifahamu mhariri. (alama 10)
- b) Fafania hali ambamo haki ulizofafania katika (a) hapo juu huruhusiwa kukiukwa. (alama 10)
4. Wewe kama mhariri wa shirika la uchapishaji la Nuru, umeipoteka kazi ya mwandishi ambaye ni mwanagenzi katika uchapishaji. Mfananulie kwa kutumia mifano majukumu yake ambaye yatachangia katika uchapishaji wa kazi yake kwa wakati ufao. (alama 20)
5. Kwa kutumia mifano, fafania majukumu yoyote sita ya mfanyikazi katika kitengo cha matbaa. (alama 20)